

Matumizi salama ya Dawa

Ninawezaje kutumia dawa yangu salama vipi?

- Fuata maagizo kwenye lebo.
- Jua wakati wa kutumia dawa yako na ni kiasi gani cha kutumia.
- Jua kiungo hai katika dawa yako.
- Orodha iliyoandikwa ya dawa zako inaweza kukusaidia, daktari wako na mfamasia wako kufuatilia dawa zako.

Ni nini kiungo hai (active ingredient)?

- Kiungo hai ndicho kinachofanya dawa yako ifanye kazi.
- Angalia lebo ili uhakikishe kuwa hauna dawa mbili au zaidi ambazo ziko tofauti lakini zina kiungo hai sawa.
- Wasiliana na daktari wako au mfamasia ikiwa una dawa zaidi ya moja ambazo zina kiungo hai sawa inayotumika.

Ninawezaje kupata kiungo hai?

- Muulize daktari wako au mfamasia wako.
- Kiungo hai kinachotumika kiko kwenye lebo.
- Weka rekodi ya kiungo hai cha dawa yako. Unaweza kuchukua picha ya dawa yako au kuweka orodha ya dawa zako.

Ninawezaje kuokoa pesa vipi kwa dawa yangu?

- Dawa zinawenza kuwa na majina tofauti - jina la kiungo hai inayotumika na jina la chapa (jina la chapa asili au jina ya chapa ya kawaida) iliopewa na mtengenezaji.
- Chapa ya kawaida mara nyingi huwa ya bei nafuu kuliko dawa ya chapa ya asili hata kama zina viungo hai sawa.
- Daktari wako au mfamasia anaweza kupendekeza upate chapa ya kawada ya dawa yako ili kuokoa pesa.

Ninaweza kugawanya dawa yangu na watu wa familia yangu au marafiki ambao pia ni wagonjwa?

- Hapana, dawa yako ni kwa ajiri yako tu.
- Inaweza kuwa hatari kwa mtu katika familia yako au rafiki ikiwa watatumia dawa yako.

Nitasimamiaje dawa zangu wakati wa janga la COVID-19?

- Tumia dawa zako kama ilivyoelekezwa na daktari wako.
- Hakikisha unazo dawa zilizoelekezwa na daktari za kutosha mwezi mmoja
- Ikiwa unahitaji kwenda hospitalini, chukua dawa zako au orodha ya dawa zako pamoja nawe.

Naweza kuzungumza na nani kuhusu dawa yangu?

- Ongea na daktari wako au mfamasia wako. Waambie ikiwa unahitaji mtafsiri.
- Pigia simu Namba ya Dawa (Medicines Line) kwa 1300 633 424. Kwa mkalimani wa simu ya bure, pigia Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service, TIS) kwa 131 450, sema lugha yako na uombe kuunganishwa na Namba ya Dawa.



Kiungo hai

